SHULE YA SEKONDARI MASHATI
S.L.P 375,
MKUU-ROMBO

Tarehe……………………………

KUMB.NA.MSTSS /J.I/F.1/VOL.1/

Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………………

S.L.P……………………………

……………………………..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASHATI WILAYA YA ROMBO MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu kuzingatia.

Kumpatia mwanafunzi ujuzi,maarifa na maadili ambayo yatamwezesha kuchukua nafasi yake katika kulitumikia Taifa lake na kumwezesha kupata mapato halali kwa kazi atakayofanya na kuwa Raia mwema.

Masomo atakayofundishwa

i.Uraia[civics]
ii.Historia[History]
iii.Jiografia[Geography]
iv.Kiswahili
v.Kiingereza[English]
vi.Hisabati[Mathematics]
vii.Kemia[Chemistry]
viii.Fizikia[Physics]
ix.Elimu yaViumbe[Biology]
X. Kompyuta [ICS]
xi. Biashara [Commerce]
xii. Uhasibu [Book keeping]
xiii..Dini[Religion]

Kwa hiyo mwanao aje na madaftari makubwa kumi na Nne [14] Counter Book 3 Quires na Daftari za Kawaida za mazoezi ya wiki kumi na Nne [14].

2.1 SARE YA SHULE:

A.WAVULANA:

i.Mashati meupe mawili ya kitambaa cha tetroni mikono mifupi.

ii.Soksi nyeusi zisizo na maua wala maandishi.

Edit with WPS Office

iii.Suruali mbili za kitambaa.

iv.T-shirt na bukta moja kwa ajili ya michezo [rangi ya bluu].

- Sare ya shule ni (ISTEM POLYSTER) Damu ya mzee .

B. WASICHANA:

i.Blausi mbili nyeupe za kitambaa cha tetroni mikono mifupi.

ii.Soksi nyeupe.

iii.Sketi mbili za kitambaa.

iv.T-shirt na bukta moja kwa ajili ya michezo [rangi ya bluu].

v.Rangi ya hijabu ifanane na Sare za Shule.

- Sare ya shule ni (ISTEM POLYSTER) Damu ya mzee .

NB:
**Kuhusu gharama za ushonaji wa sare ya shule wazazi watakubaliana na fundi siku ya kikao tarehe 11/01/2021.**

C.WAVULANA NA WASICHANA:
Viatu vyeusi [visivyo na kisigino kirefu vya kufunga kwa Kamba pia mabuti hayaruhusiwi].
Sweta moja ,begi la ngozi au turubali la kubebea vifaa vya shule [mifuko ya nailoni hairuhusiwi]. Wote waje na Mathematical set na folder file moja yenye Kamba zake,pamoja na picha 1 passport size.

2.2 MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU

Shule ya sekondari Mashati hutoa huduma nyingine za uji pamoja na Chakula cha mchana kwa wanafunzi baada ya Makubaliano ya Wazazi wenyewe kwenye Vikao vyao kama inavyoelezwa katika waraka wa Elimu namba 3wa mwaka 2016.

ANGALIZO:
1.VIAMBATANISHO 1,2 viletwe shuleni vikiwa vimejazwa kwa usahihi na wahusika.
2.Mzazi/Mlezi atakayemshonea mtoto wake suruali,sketi au blausi kwa kutozingatia maagizo ya sampuli za kitambaa na mtindo wa ushonaji,mwanae hatapokelewa shuleni.
NB.Siku ya kuripoti shuleni mwanafunzi afike na mzazi/mlezi wake.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

E. C. Mrosso

MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

Simu Na.+255272756455

.

SHULE YA SEKONDARI MASHATI
Mobile no.+255752847062 S.L.P 375
E-mail:mashatisecschool@yahoo.com MKUU-ROMBO.

KIAMBATANISHO NA. 2

YAH: FOMU YA KUKUBALI/KUTOKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASHATI.

1. MWANAFUNZI

   Mimi mwanafunzi: …………………………………………………………………………….[Jina la mwanafunzi]

   Nakiri kuwa nimesoma na kuelewa yote yaliyoko kwenye maagizo ya kujiunga na shule hii,na nitayazingatia kwa muda wangu wote wa masomo yangu hapa shuleni.

   ……………………………………. …………………………..

   SAHIHI TAREHE

2. MZAZI/MLEZI:

   Mimi ………………………………………………………………… [Jina kamili] ambaye ni mzazi/mlezi wa

   ……………………………………………………… [Jina la mtoto anayejiunga]

   Nakiri kupokea ,kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizoko kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya Sekondari Mashati.Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakua tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mwanangu anayejiunga na shule hii.

   ……………………………………….. ……………………………….
   .

   SAHIHI TAREHE

Edit with WPS Office

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

ROMBO DISTRICT COUNCIL

MASHATI SECONDARY SCHOOL

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

APPENDEX I:

To be completed by a Medical Officer in Government Hospital in respect of all new entrants to Mashati Secondary School.

Full Name:……………………………………………………………………………

Age:……………….

1.Blood count [red & white] ……………………………………………………………………………………………………

2.Stool examination: ………………………………………………………………………………………………………………

3.Urine examination: ……………………………………………………………………………………………………………

4.Eye test: ……………………………………………………………………………………………………………………………

5.Ear test: ……………………………………………………………………………………………………………………………

6.T.B test: ……………………………………………………………………………………………………………………………

7.STDs test: …………………………………………………………………………………………………………………………

8.Spleen: ……………………………………………………………………………………………………………………………

9.Abdomen:…………………………………………………………………………………………………………………………

10.Additional information from any physical, mental, hereditary diseases or disabilities

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

Edit with WPS Office

11. Speech test: ……………………………………………………………………………………………………………………………….

Treatment after examination: ……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………………….

Please state nature of treatment………………………………………………………………………………………………

Medical Certificate.

I certify that the above mentioned name has been examined and found fit to pursue further Education.

Signature: …………………………………………………

Designation: …………………………………………….

Date: …………………………………………………….…     Station: …………………………………….

# OFISI YA RAISI

# TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

# SHULE YA SEKONDARI MASHATI


SIMU NA: 027-2756455
0752-847062

SHULE YA SEKONDARI MASHATI
S.L.P. 375
MKUU - ROMBO.


## 6. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII:

### A. WAJIBU WA MWANAFUNZI ANAYESOMA SEKONDARI

i. Kuwa na heshima kwa walimu, watumishi wengine wote waliomzidi umri na wadogo.
ii. Kuogea lugha safi isiyo na maasi wala kashfa kwa binadamu yeyote awaye.
iii. Kushiriki na kusaidiana katika kazi za shule.
iv. Kuwahi shule, kufanya kazi zote za shule kuendana na maagizo yatolewayo na uongozi wa shule.
v. Kuhakikisha kwamba mazingira ya shule anamoishi yanakuwa safi wakati wote kwa kufanyia usafi.

Edit with WPS Office

vi. Kusimama na kusalimia wakubwa wanapopita mbele yake.
vii. Kupokea kwa heshima mizigo kwa watumishi wa shule na wageni wa shule na kuwasaidia.
viii. Kuheshimu Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, Nembo ya Taifa, Fedha za Taifa, picha za viongozi wa Serikali n.k.
ix. Kusimama kusalimia kwa heshima mwalimu/walimu mara tu aingiapo /waingiapo darasani.
x. Kutii na kuheshimu wito wowote unaotolewa shuleni.
xi. Kutii na kuheshimu wito wa kengele inapogongwa
xii. Kuheshimu mahali pa mikusanyiko kwa utulivu na kufuata utaratibu uliowekwa
xiii. Kuheshimu na kutunza mali za umma na binafsi
xiv. Kusoma kwa bidii na kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa shuleni na Taifa.
xv. Kulipa ada na michango mingine ya shule bila kuchelewa
xvi. Kufuata sheria zote za shule.

B. <u>MAMBO AMBAYO HAYARUHUSIWI MWANAFUNZI KUYATENDA</u>

i. Kutumia tumbaku au ulevi wa aina yoyote
ii. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
iii. Kufuga kucha , ndevu, na kuvaa hereni , bangili,mikufu na viwalo tofauti na sare ya shule.
iv. Kuiga mitindo ya kihuni k.m. kunyoa kipara, panki, kupaka midomu rangi na kucha, marashi n.k.
v. Kutumia lugha ya matusi au kashafa.
vi. Kupigana au kupiga mtu, wizi, kugoma/kukataa adhabu, kutishia, kushawishi / kushiriki kugoma
vii. Kutoroka vipindi darasini
viii. Kutoka nje ya maeneo ya shule bila ruksa kutoka kwa mwalimu mhusika
ix. Kutembelea maeneo k.m. vilabu vya pombe, majumba ya starehe, nyumba za kufikia wageni [guest house] nyumba za watumishi, ofisi za walimu bila ruksa, kufanya uasherati,ushoga n.k.
x. Kupata au kusababisha mimba
xi. Kupatikana na kosa la jinai
xii. Kuharibu mali ya umma au ya binafsi.

NB:MWANAFUNZI AKIENDA KINYUME NA YALIYOKWISHA TAJWA HAPO JUU HATUA ZA KINIDHAMU ZITACHUKULIWA DHIDI YAKE.

C. <u>MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE</u>

i. Wizi

Edit with WPS Office

ii. Uasherati, ubakaji, kulawiti, na ushoga
iii. Ulevi wa pombe,matumizi ya madawa ya kulevya k.m.bangi n.k.
iv. Makosa ya jinai
v. Kupigana au kumpiga mtu
vi. Kuharibu mali ya umma / mali ya mtu binafsi.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata au kusababisha mimba.
x. Kutoa /kuharibu , kusaidia kutoa au kuharibu mimba.
xi. Kugoma , kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu
xii. Kukataa adhabu, kutoheshimu watu wenye mamlaka dhidi yake
xiii. Kukutwa na simu ya mkononi [mobile phone] shuleni.

7. MAMBO MENGINE MUHIMU [VIAMBATANISHO]

i. KIAMBATANISHO NA.I: MEDICAL EXAMINATION FORM
Fomu hii ijazwe kikamilifu na Mganga Mkuu wa Hospitali/Kituo cha Afya cha Serikali na kukabidhiwa kwa Mkuu wa shule siku mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

ii. KIAMBATANISHO NA.2: STUDENT HISTORY SHEET.
Fomu hii ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa mwanafunzi wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai ijazwe na kuwasilishwa kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni.

iii. KIAMBATANISHO NA.3:
FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASHATI.

Fomu hii ijazwe kwa makini na Mzazi/Mlezi na mwanafunzi baada ya kusoma na kuelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na kuiwasilisha kwa Mkuu wa shule tarehe ya kuripoti shuleni.

ANGALIZO:

NB: MWANAFUNZI ASIYETEKELEZA MAAGIZO NA MAELEZO YA BARUA HII HATAPOKELEWA SHULENI.

*NAKUTAKIA KILA LA KHERI NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII*

Edit with WPS Office